**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

# BAJETI YA SERIKALI YA MWAKA 2024/25
# KWA LUGHA RAHISI
# TOLEO LA MWANANCHI

**Yaliyomo**


1. UTANGULIZI ........................................................................1
2. SHABAHA ZA UCHUMI JUMLA ..............................................2
3. MISINGI YA BAJETI ..........................................................2
4. VIPAUMBELE VYA BAJETI YA MWAKA 2024/25 ........................3
5. JE, SERIKALI INATARAJIA KUKUSANYA MAPATO KUTOKA VYANZO VIPI?........................................................................3
6. JE, MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/25 NI YAPI? ....4
7. MGAWANYO WA MATUMIZI KWA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA ..........................................................................5
8. MATUMIZI YA SERIKALI KISEKTA..........................................6
9. MABORESHO YA MFUMO WA KODI, ADA, TOZO NA HATUA NYINGINE ZA MAPATO..........................................15

## 1. Utangulizi


Bajeti ya Serikali ni mpango unaoonesha namna Serikali itakavyokusanya na kutumia fedha katika kipindi cha mwaka mmoja kwa kuzingatia vipaumbele vya nchi. Kupitia bajeti, Serikali inapanga kutumia mapato kutoka katika vyanzo mbalimbali yatakayokusanywa kwa ajili ya kugharamia utoaji wa huduma kwa wananchi kama vile elimu, afya, maji na barabara.

Bajeti ya Serikali Toleo la Mwananchi ni kijitabu kinachoandaliwa kwa lugha rahisi inayoeleweka kwa wananchi na wadau wote. Kijitabu hiki kinatoa taarifa za msingi kuhusu mapato na matumizi ya Serikali, vipaumbele vya kisekta pamoja na sera za uchumi jumla kwa mwaka husika wa fedha. Dhumuni la toleo hili la bajeti ni kuongeza uwazi, uwajibikaji na ushiriki wa wananchi katika mchakato mzima wa bajeti ya Serikali.

Aidha, dhima kuu ya Bajeti ya Mwaka 2024/25 kama ilivyokubaliwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni "*Mageuzi Endelevu ya Kiuchumi kupitia Uimarishaji wa Sera za Kibajeti na Uwekezaji katika Kuhimili na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kwa Maendeleo ya Wananchi*"

### 1.1 Mchakato wa Bajeti ya Serikali

Mchakato wa bajeti ya Serikali ni mzunguko endelevu wa mwaka mzima, kuanzia hatua ya uandaaji na uidhinishwaji wa Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti hadi utekelezaji wake. Kielelezo kifuatacho kinaonesha mchakato wa Bajeti ya Serikali.



## 2. Shabaha za Uchumi Jumla



Ukuaji wa Pato la Taifa kufikia asilimia 5.4 mwaka 2024 kutoka ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2023





Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati



Mapato ya ndani kufikia asilimia 15.8 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 15.4 mwaka 2023/24



Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.9 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 ikilinganishwa matarajio ya asilimia 12.6 mwaka 2023/24




Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4)



Kuwa na nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa.

## 3. Misingi ya Bajeti

Uandaaji wa shabaha za uchumi jumla kwa mwaka 2024/25 umezingatia misingi ifuatayo:

i. Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara;
ii. Kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, vita, magonjwa ya mlipuko, mafuriko;
iii. Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa;
iv. Kuendelea kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini; na
v. Uwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani.

## 4. Vipaumbele vya Bajeti ya Mwaka 2024/25

Serikali itaendelea kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ambavyo vimegawanyika katika maeneo matano. Maeneo hayo ni: Kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kukuza uwekezaji na biashara, kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza rasilimali watu.

Kwa mwaka 2024/25, Serikali itaendelea kukamilisha miradi ya kielelezo na kimkakati, kuimarisha sekta za uzalishaji, kuimarisha rasilimali watu hususani katika sekta za huduma za jamii, kuongeza matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Serikali, na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji wa sekta binafsi. Aidha, maeneo mengine ya muhimu katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/25 ni kugharamia mishahara ya watumishi wa umma, deni la Serikali, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024, maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, na maandalizi ya michuano ya mpira wa miguu ya mataifa ya Afrika (AFCON) ya mwaka 2027 ikiwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa viwanja.

## 5. Je, Serikali inatarajia kukusanya mapato kutoka vyanzo vipi?

Serikali inatarajia kukusanya mapato jumla ya shilingi trilioni 49.35 kwa ajili ya kugharamia matumizi yake. Mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani yanakadiriwa kuwa shilingi trilioni 34.61 na mapato kutoka vyanzo vya nje ikiwemo misaada na mikopo ni shilingi trilioni 14.74.

### 5.1 Mikakati ya Kuongeza ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuongeza mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa kibajeti na kuchochea maendeleo ya Taifa letu. Hatua hizo ni pamoja na:

i. Kuendelea kuhimiza matumizi ya **Kumbukumbu Namba ya Malipo (*Control Number*)** katika kufanya malipo yote ya Serikali ili kudhibiti upotevu wa mapato;

ii. Serikali itaendelea kuboresha vyanzo vya mapato kwa kuhakikisha vinaakisi misingi ya ukusanyaji mapato;

iii. Utoaji elimu kwa umma kuhusu ulipaji kodi utakuwa endelevu ili kuongeza uhiari wa kulipa kodi na kuhakikisha kodi stahiki inakusanywa;

iv. Serikali itaendelea kutambua walipakodi wapya ikiwemo kusajili kampuni za kimataifa zinazoendesha biashara

kidijitali hapa nchini kupitia mfumo wa usajili uliorahisishwa;

v. Serikali inaendelea kufanya maboresho ya mifumo ya taasisi zinazotoa huduma zinazohusiana ili kutoa ankara jumuishi ya malipo itakayorahisisha upatikanaji wa mapato kwa wakati na kupunguza muda wa utoaji wa huduma kwa wananchi;

vi. Serikali imeendelea kuwekeza kwenye matumizi ya TEHAMA ili kuhakikisha mifumo ya Serikali inabadilishana taarifa kwa urahisi na usahihi, kuondoa urudufu na kuimarisha ufuatiliaji na usimamizi wa fedha za umma;

vii. Serikali inakusudia kuanzisha Tuzo ya Uzalendo kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Risiti za Kielektroniki ili kuhamasisha tabia ya wananchi kudai risiti stahiki pindi wanapofanya manunuzi, na wafanyabiashara kutoa risiti kwa hiari pale wanapofanya mauzo; na

viii. Serikali kuendelea kuongeza juhudi za kuboresha mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara na uwekezaji kwa kurahisisha taratibu na kanuni za uanzishaji na uendeshaji.




**6. Je, matumizi ya Serikali kwa mwaka 2024/25 ni yapi?**

Katika mwaka 2024/25 Serikali inatarajia kutumia shilingi trilioni 49.35 kugharamia mahitaji mbalimbali ikiwemo:

i. Mishahara ya watumishi shilingi trilioni 11.77;

ii. Malipo ya riba shilingi trilioni 5.58;

iii. Malipo ya mtaji shilingi trilioni 7.54;

iv. Miradi ya maendeleo inayogharamiwa na fedha za ndani shilingi trilioni 12.32;

v. Miradi ya maendeleo inayogharamiwa na fedha za nje shilingi trilioni 3.64; na

vi. Undeshaji wa shughuli za Serikali shilingi trilioni 8.50.

### 6.1 Hatua za Usimamizi wa Matumizi ya Fedha Za Umma

i. Kuimarisha uwajibikaji na udhibiti katika matumizi ya fedha za umma kwa kusimamia utekelezaji wa sheria, miongozo na nyaraka mbalimbali za Serikali;

ii. Kuendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa shughuli za Serikali ikijumuisha mifumo ya usimamizi wa rasilimali watu, malipo serikalini, ununuzi wa umma na usimamizi wa mali za Serikali;

iii. Kuimarisha usimamizi wa taratibu za ununuzi wa umma ili kuhakikisha ununuzi wa umma unakuwa wenye tija na kuendana na thamani ya fedha;

iv. Kupunguza safari za ndani na nje na kupunguza ukubwa wa uwakilishi kwenye mikutano ya ndani na nje ya nchi;

v. Kuendelea kutekeleza Mkakati wa Kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa Kutumia Vyanzo Mbadala ili kupunguza utegemezi wa bajeti ya Serikali Kuu; na

vi. Kuimarisha vitengo vya ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha shughuli zinazotekelezwa zinaakisi thamani halisi ya fedha.

## 7. Mgawanyo wa Matumizi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

Baadhi ya maeneo yaliyopewa kipaumbele katika matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ni:

i. Shilingi bilioni 401.6 kwa ajili ya Elimu Bila Ada kwa shule za msingi na sekondari;

ii. Shilingi bilioni 243.9 kwa ajili ya usimamizi wa mitihani ya Kitaifa;

iii. Shilingi bilioni 17.9 kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi viporo na maboma ya vyumba vya madarasa vilivyojengwa na wananchi, mabwalo na mabweni katika shule za msingi na sekondari;


iv. Shilingi bilioni 64.8 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya utawala, nyumba za Wakurugenzi na Wakuu wa Idara;

v. Shilingi bilioni 68.8 kwa ajili ya ukamilishaji wa hospitali za wilaya, vituo vya afya, zahanati pamoja na ukarabati wa hospitali kongwe za halmashauri; na

vi. Shilingi bilioni 36.2 kwa ajili ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo.

Aidha, Serikali imetenga shilingi bilioni 541.27 fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu ya afya, elimu, utawala na uchumi.

## 8. Matumizi ya Serikali Kisekta




### 8.1 Sekta ya Elimu

Sekta ya Elimu imetengewa shilingi trilioni 6.16[1] katika maeneo ya vipaumbele kama ifuatavyo:-

i. Shilingi trilioni 4.39 kwa ajili ya elimu ya awali, msingi na sekondari, vyuo vya ualimu, ukaguzi wa shule, elimu ya watu wazima na elimu isiyo rasmi;

ii. Shilingi trilioni 1.34 kwa ajili ya elimu ya juu, sayansi na teknolojia ikijumuisha shilingi bilioni 787.4 kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu;

iii. Shilingi bilioni 196.53 kwa ajili ya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi;

iv. Shilingi bilioni 157.18 kwa ajili ya matumizi ya utawala; na

v. Shilingi bilioni 72.37 kwa ajili ya Sayansi na Teknolojia.




[1] Kiasi hiki hakijumishi shilingi bilioni 66.55 ya vyuo katika sekta mbalimbali

## 8.2 Sekta ya Afya

Sekta hii imetengewa jumla ya shilingi trilioni 2.54. Baadhi ya maeneo ya kipaumbele ni kama ifuatavyo:


i. Shilingi trilioni 1.06 kwa ajili ya kuboresha huduma za tiba na miundombinu katika hospitali za rufaa ngazi ya kanda na taifa;

ii. Shilingi bilioni 901.82 kwa ajili ya kuboresha huduma na miundombinu ya afya katika hospitali za wilaya;

iii. Shilingi bilioni 310.73 kwa ajili ya huduma za kinga ikiwemo ununuzi na usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo;

iv. Shilingi bilioni 170.27 kwa ajili ya kuboresha huduma na miundombinu ya afya katika zahanati na vituo vya afya; na

v. Shilingi bilioni 95.65 kwa ajili ya kugharamia shughuli za utawala na rasilimali watu katika utoaji wa huduma za afya.




## 8.3 Sekta ya Hifadhi ya Jamii

Serikali imetenga shilingi trilioni 2.65 kwa ajili ya Sekta ya Hifadhi ya Jamii. Baadhi ya shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: kuwezesha makundi maalum hususan wafanyabiashara wadogo wakiwemo machinga, mama/baba lishe, waendesha bodaboda na bajaji kupitia utoaji wa mikopo; kuimarisha uhai na ustahimilivu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa watoto na wazee; kuimarisha miundombinu katika vyuo vya maendeleo ya jamii; na kukarabati na kujenga vituo vya wazee na shule za watoto za maadilisho.

### 8.4 Sekta ya Ulinzi, Usalama na Utii wa Sheria

Sekta hii imetengewa jumla ya shilingi trilioni 5.49. Baadhi ya maeneo ya kipaumbele ni kama ifuatavyo:-

i. Shilingi trilioni 3.32 kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa Taifa;
ii. Shilingi trilioni 1.70 kwa ajili ya kudumisha amani na usalama wa raia na mali zao; na
iii. Shilingi bilioni 465.89 kwa ajili ya kuimarisha utawala wa Sheria.

### 8.5 Sekta ya Huduma za Utawala na Deni la Serikali

Sekta hii imetengewa shilingi trilioni 13.23 kugharamia shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:

i. Shilingi trilioni 5.58 kwa ajili ya kugharamia malipo ya riba;
ii. Shilingi trilioni 5.06 kwa ajili ya shughuli za utawala;
iii. Shilingi trilioni 2.34 kwa ajili ya shughuli za fedha na uchumi ikijumuisha shilingi bilioni 167.1 za maandalizi ya uchaguzi mkuu 2025; na
iv. Shilingi bilioni 240.75 kwa ajili ya shughuli za mambo ya nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

### 8.6 Sekta ya Maendeleo ya Uchumi

#### 8.6.1 Sekta ya Kilimo

Katika mwaka wa fedha 2024/25, Sekta ya Kilimo ambayo inajumuisha mifugo na uvuvi imetengewa jumla ya shilingi trilioni 1.93 kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa shughuli muhimu zitakazowezesha mapinduzi ya kilimo kuwa chenye tija na kinachowanufaisha wakulima. Baadhi ya maeneo ambayo matumizi yameelekezwa ni pamoja na:

i. Shilingi bilioni 230.0 kwa ajili ya ruzuku ya mbolea kwa msimu wa kilimo wa 2024/25;
ii. Shilingi bilioni 70.0 kwa ajili ya kuiwezesha Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC); kununua na kusambaza mbolea kwenye maeneo yasiyovutiwa na soko;
iii. Shilingi bilioni 40.7 kwa ajili ya kununua pembejeo za zao la korosho;
iv. Shilingi bilioni 36.2 kwa ajili ya kuwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kununua tani 100,000 za chakula ili kuongeza usalama wa chakula nchini;
v. Shilingi bilioni 10.0 kwa ajili ya kuwezesha Mfuko wa Pembejeo kutoa mikopo kwa wakulima (vijana na wanawake);

vi. Shilingi bilioni 34.9 kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu na miche bora ya kilimo;

vii. Shilingi bilioni 32.1 kwa ajili ya shughuli za utafiti wa kilimo;

viii. Shilingi bilioni 28.5 kwa ajili ya utekelezaji wa programu ya jenga kesho iliyo bora (BBT) ikiwa ni pamoja na kilimo cha umwagiliaji kwenye mashamba makubwa;

ix. Shilingi bilioni 150.0 kwa ajili ujenzi wa bandari ya uvuvi ya Kilwa;

x. Shilingi bilioni 28.1 kwa ajili ya kuiwezesha Wakala wa Maabara za Mifugo Tanzania (TVLA) kuboresha maabara zake na upatikanaji wa chanjo muhimu 13 za mifugo;

xi. Shilingi bilioni 13.8 kwa ajili ya kuboresha hekta 20,000 za malisho na chakula cha mifugo pamoja na kuanzisha kambi maalum ya kuongeza thamani ya mifugo katika ranchi ya Mkata;

xii. Shilingi bilioni 25.9 kwa ajili ya ununuzi wa boti za uvuvi 180 pamoja na vifaa vya uvuvi na kujenga masoko na mialo ya samaki;

xiii. Shilingi bilioni 92.9 kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa mapya 100 na kumalizia ujenzi wa mabwawa 14 unaoendelea;

xiv. Shilingi bilioni 87.5 kwa ajili ya kugharamia ujenzi unaoendelea wa skimu 53 zenye jumla ya hekta 202,257.46 pamoja na mashamba makubwa ya pamoja chini ya programu ya jenga kesho iliyo bora; na

xv. Shilingi bilioni 20.5 kwa ajili ya kuanza uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye mabonde 22 yenye jumla ya hekta 306,361.




### 8.6.2 Sekta ya Nishati

Sekta hii imetengewa shilingi trilioni 1.88 ili kutekeleza vipaumbele mbalimbali ikiwemo:

i. Shilingi bilioni 659.0 kwa ajili ya miradi ya kuzalisha umeme ikijumuisha shilingi bilioni 620.0 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Bwawa la Julius Nyerere Megawati 2115;
ii. Shilingi bilioni 11.0 kwa ajili ya uzalishaji na usambazaji nishati safi ya kupikia;
iii. Shilingi bilioni 200.0 kwa ajili ya ukarabati na uboreshaji wa Gridi ya Taifa;
iv. Shilingi bilioni 350.0 kwa ajili ya usambazaji umeme vijijini;
v. Shilingi bilioni 254.0 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha, kusambaza na kupoza umeme; na
vi. Shilingi bilioni 61.0 kwa ajili ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati na ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza gesi asilia na mafuta.

### 8.6.3 Sekta ya Madini

Kwa kutambua umuhimu wa mchango wa Sekta ya Madini katika kukuza uchumi wa Taifa, Serikali imetenga shilingi bilioni 231.90 kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele mbalimbali ikiwemo: uendelezaji wa madini muhimu na madini mkakati kwa kufanya utafiti wa mahitaji ya madini hayo ili kuyafikia masoko mbalimbali duniani na kuvutia wawekezaji; uongezaji thamani madini kwa kutengeneza bidhaa zitokanazo na madini ghafi; uanzishwaji wa minada na maonesho ya madini ya vito; kuendelea kufanya utafiti na ugani wa jiosayansi ikiwemo utafiti wa kina wa jiofizikia; kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kutoa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu masuala muhimu ya kuzingatia katika uendeshaji wa shughuli za madini, kuwatengea maeneo pamoja na kuimarisha miundombinu na utendaji wa vituo vya kuwapa huduma.

### 8.6.4 Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Katika bajeti ya mwaka 2024/25, Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imetengewa jumla ya shilingi trilioni 5.48 kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele mbalimbali. Mchanganuo wa bajeti kwa ajili ya baadhi ya vipaumbele ni kama ifuatavyo:

#### 8.6.4.1 Ujenzi

i. Shilingi trilioni 1.52 kwa ajili ya ujenzi wa barabara na madaraja;
ii. Shilingi bilioni 599.0 kwa ajili ya matengenezo ya barabara kupitia Mfuko wa Barabara;
iii. Shilingi bilioni 24.8 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vivuko;
iv. Shilingi bilioni 28.2 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya Serikali na Nyumba za Viongozi kupita Wakala wa Majengo Tanzania;

v. Shilingi bilioni 4.01 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa karakana za Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA);
vi. Shilingi bilioni 48.5 kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya Mzunguko wa Nje katika Jiji la Dodoma;
vii. Shilingi bilioni 109.7 kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege; na
viii. Shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya maandalizi ya awali ya ujenzi wa Barabara ya Dar es Salaam - Kibaha – Chalinze – Morogoro – Dodoma Expressway yenye urefu wa kilometa 531.8, mradi unaotekelezwa kwa utaratibu wa ushirikiano wa Sekta binafsi na Sekta ya Umma.

**8.6.4.2 Uchukuzi**

i. Shilingi trilioni 1.51 kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR);
ii. Shilingi bilioni 294.8 kwa ajili ya Mfuko wa Reli (RIF);
iii. Shilingi bilioni 82.8 kwa ajili ya shughuli za uendeshaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC);
iv. Shilingi trilioni 1.8 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA);
v. Shilingi bilioni 98.7 kwa ajili ya kusimamia ubora wa huduma za usafiri wa anga kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA);
vi. Shilingi bilioni 161.2 kwa ajili ya kugharamia uendeshaji na uwekaji miundombinu ya viwanja vya ndege nchini (TAA);
vii. Shilingi bilioni 324.5 kwa ajili ya ununuzi na ukarabati wa ndege (ATCL); na
viii. Shilingi bilioni 15.9 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na mundombinu ya rada na hali ya hewa nchini (TMA).

**8.6.4.3 Mawasiliano**

i. Shilingi bilioni 80.0 kwa ajili ya mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; na
ii. Shilingi bilioni 11.5 kwa ajili ya mradi wa Mfumo wa Anwani za Makazi nchini.

### 8.6.5 Sekta ya Viwanda na Biashara

Katika mwaka 2024/25, Sekta ya Viwanda na Biashara imetengewa jumla ya shilingi bilioni 383.15 kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele vya kujenga na kuimarisha misingi thabiti ya uchumi ikiwemo kuvutia uwekezaji na kujenga uchumi wa viwanda. Vipaumbele vikuu vya sekta ni: kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati; kuimarisha uwezo wa uzalishaji

viwandani na utoaji huduma kwa kuimarisha miundombinu na mazingira wezeshi; kuboresha mazingira ya biashara; kuchochea maendeleo ya watu kwa kuboresha miradi na programu katika sekta ya jamii inayohusisha elimu na mafunzo ya ujuzi; kuendelea na utafutaji wa masoko kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini; na kuchochea ukuaji wa Sekta binafsi nchini. Pamoja na kuendeleza: miradi ya kimkakati ya Magadi Soda Engaruka na Makaa ya mawe Mchuchuma na Chuma cha Liganga; kiwanda cha Kilimanjaro Machine Tools Company (KMTC); na utengenezaji wa kibiashara wa viwanda vidogo vya kuchakata sukari (sugar mill mini-processing plant - Capacity 200 TCD).

### 8.6.6 Sekta Ya Maliasili , Utalii na Mazingira

Katika mwaka 2024/25, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 335.35 kwa ajili ya kuendeleza sekta ya utalii nchini na kuendelea kutekeleza vipaumbele vya shughuli za kuhifadhi, kutunza na kusimamia maliasili na mazingira.

### 8.6.7 Sekta ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Kukuza Ujuzi

Katika mwaka 2024/25, sekta hii imetengewa shilingi bilioni 33.99 kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele mbalimbali ikiwemo:

i. Shilingi bilioni 10.81 kwa ajili ya Mradi wa Kuunganisha wahitimu na mafunzo ya uzoefu kazini;
ii. Kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi nchini, kufanya kaguzi katika maeneo ya kazi na kuridhia mikataba ya Shirika la Kazi Duniani;
iii. Kufanya kaguzi, kupima afya za wafanyakazi na kutoa mafunzo kwa waajiri na wafanyakazi na wajasiriamali wapatao 38,000 kwa lengo la kuendelea kusimamia sheria ya usalama na afya mahali pa kazi;
iv. Kuhuisha Sera ya Ajira ya Mwaka 2008 pamoja na kuweka mazingira bora ya kisheria ya kuratibu uzalishaji wa fursa za ajira na kukuza ujuzi;
v. Kuimarisha ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za soko la ajira nchini;
vi. Kutoa mafunzo kwa watanzania kuhusu kushindania fursa za ajira nje ya nchi na kuwaunganisha na fursa hizo;
vii. Kusimamia masuala ya malezi na makuzi kwa vijana nchini; na
viii. Kuwawezesha vijana kiuchumi kwa kutoa mikopo ili waweze kujiajiri na kutengeneza fursa za ajira kwa vijana wenzao.

## 8.7 Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Sekta hii imetengewa shilingi trilioni 1.42 kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali.

### 8.7.1 Sekta ya Ardhi

Kwa mwaka 2024/25, sekta hii imetengewa shilingi bilioni 174.19 kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za kipaumbele. Miongoni mwa vipaumbele hivyo ni:

i. Shilingi bilioni 55.9 kwa ajili ya uboreshaji wa milki za ardhi;
ii. Shilingi bilioni 6.1 kwa ajili ya uimarishaji wa miundombinu ya upimaji na ramani;
iii. Shilingi bilioni 19.4 kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi;
iv. Shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya uimarishaji wa mipaka ya kimataifa; na
v. Shilingi bilioni 5.0 kwa ajili ya mipango ya matumizi bora ya ardhi.

### 8.7.2 Sekta ya Maendeleo ya Jamii

Katika mwaka 2024/25, Sekta ya Maendeleo ya Jamii imetengewa jumla ya shilingi bilioni 320.31 kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele mbalimbali kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Baadhi ya maeneo ya vipaumbele ni kama vifuatavyo: -

i. Shilingi bilioni 266.91 imetengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya jamii katika halmashauri;
ii. Shilingi bilioni 3.2 kwa ajili ya kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi;
iii. Shilingi bilioni 3.2 kwa ajili ya kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto;
iv. Shilingi bilioni 10.5 kwa ajili ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu ili kuongeza mitaji na kuboresha shughuli za kiuchumi za makundi maalum na wafanyabiashara wadogo;
v. Shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya huduma za ustawi wa jamii na watoto ikiwa ni pamoja na utoaji wa huduma za marekebisho ya tabia kwa watoto waliokinzana na sheria;
vi. Shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma katika makazi 13 ya wazee;
vii. Shilingi bilioni 2.0 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa taasisi na vyuo vya maendeleo ya jamii; na
viii. Shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

### 8.7.3 Sekta ya Maji

Katika mwaka 2024/25, Serikali imetenga shilingi bilioni 641.88 kwa ajili ya sekta ndogo ya maji ili kutekeleza shughuli mbalimbali za kipaumbele ikiwemo miradi ya kusambaza maji mijini na vijijini. Baadhi ya miradi ya kipaumbele ni pamoja na:

i. Shilingi bilioni 226.0 kwa ajili ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini;
ii. Shilingi bilioni 246.65 kwa ajili ya mradi wa kukarabati miundombinu na kusambaza maji Mijini;
iii. Shilingi bilioni 37.02 kwa ajili ya mradi wa kusimamia na kuendeleza rasilimali maji;
iv. Shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya usimamizi wa huduma ya ubora wa maji; na
v. Shilingi bilioni 37.8 kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji safi kutoka ziwa Victoria kwenda mkoa wa Simiyu na kukamilisha usanifu wa kupeleka maji katika Mikoa ya Singida na Dodoma.

### 8.7.4 Sekta ya Habari, Michezo na Utamaduni

Katika mwaka 2024/25, Serikali imetenga shilingi bilioni 285.29 kwa ajili ya kukuza na kuendeleza sekta ya habari, michezo na utamaduni. Maeneo ya vipaumbele ni pamoja na;-

i. Ujenzi na ukarabati wa viwanja ikiwemo kiwanja cha michuano ya Mpira wa Miguu ya Mataifa ya Afrika (AFCON) ya mwaka 2027;
ii. Kufungua vituo 100 vya ufundishaji Kiswahili kote Duniani kwa kushirikiana na Diaspora, lengo ni kukuza, kueneza na kubidhaisha zaidi Kiswahili;
iii. Kuimarisha utoaji wa mikopo na ruzuku kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania;
iv. Kufanya tafiti za kutambua mchango wa sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo katika uchumi;
v. Ujenzi wa akademia 10 za kulea vipaji katika shule maalumu za michezo; na
vi. Kutunga kanuni za uwazi za fedha kwa vyama na mashirikisho ya michezo.

## 9. Maboresho ya Mfumo wa Kodi, Ada, Tozo na Hatua Nyingine za Mapato

Serikali imefanya maboresho mbalimbali katika mifumo ya kodi, ada kupitia marekebisho ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2024. Baadhi ya maboresho hayo ni kama ifuatavyo:

### a. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), SURA 148

i. Serikali imetoa msameha wa VAT kwenye madawa ya kutibu na kusafisha maji, dira za maji na huduma ya uondoshaji wa maji taka ili kufanikisha utoaji wa huduma ya maji safi na salama nchini;

ii. Serikali imetoa msamaha kwenye vifaa na mitambo ya kuchakata na kuhifadhi mazao ya nyuki ili kukuza sekta ndogo ya nyuki nchini;

iii. Serikali imetoa msamaha wa VAT kwenye uingizwaji wa vifaa vya kiteknolojia kwa ajili ya kuwasaidia waamuzi ili kuhakikisha nchi inapata vifaa muhimu vya michezo kwa kuzingatia kuwa, Tanzania ni moja ya nchi mwenyeji zitakazohusika katika maandalizi ya michuano ya fainali ya kuwania kombe la mataifa ya Afrika (AFCON) mwaka 2027;

iv. Serikali imeondoa msamaha wa VAT kwenye chepe na sururu ambavyo vilijumuishwa kwenye msamaha wa vifaa vya kilimo ili kupunguza misamaha isiyo na tija kwa lengo la kulinda mapato ya Serikali;

v. Serikali itatoza VAT kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye madini ya dhahabu yatakayouzwa kwa Benki Kuu ya Tanzania, kwa viwanda vya kusafishia dhahabu nchini na kufuta msamaha wa VAT kwenye madini ya thamani, madini ya vito na madini mengine ya thamani yanayouzwa kwenye vituo vya kusafishia dhahabu vilivyopo nchini. Lengo la hatua hizi ni kuongeza mchango wa Sekta ya Madini katika ukuaji wa Pato la Taifa, kuipa Serikali akiba ya fedha za kigeni na kuwezesha madini ghafi ya dhahabu yanasafishwa nchini na kuongezewa thamani kabla ya kusafirishwa kwenda nje ya nchi;

vi. Serikali itatoza VAT kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye mbolea inayozalishwa ndani ya nchi kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuleta unafuu kwa wakulima na walaji hasa katika kipindi hiki cha mdororo wa uchumi duniani;

vii. Serikali itatoza VAT kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye bidhaa za nguo zinazotengenezwa kwa kutumia pamba inayolimwa nchini na kwenye mbolea inayozalishwa ndani ya nchi kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuleta unafuu kwa wakulima wa pamba na viwanda vinavyotengeneza

nguo nchini hasa katika kipindi hiki cha mdororo wa uchumi;

viii. Serikali imesamehe VAT kwenye mafuta ya kula yanayozalishwa ndani ya nchi kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini kwa muda wa mwaka mmoja ili kuendeleza unafuu wa bei ya mafuta ya kula iliyopanda kutokana na mdororo wa uchumi pamoja na vita ya Urusi na Ukraine vilivyosababisha uhaba wa mafuta hayo; na

ix. Serikali itatoza VAT kwenye huduma ya *data* zinazotolewa mtandaoni (online data service) sambamba na kuweka tafsiri ya maneno *online data services* na kujumuisha huduma hiyo kwenye wigo wa utozaji wa huduma za kidijitali ili kuongeza wigo wa kodi na kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia.

Hatua zote hizo katika kodi ya VAT kwa ujumla wake zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 22.39**.**

### b. Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332

Serikali imeweka takwa la risiti za kielektroniki kutumika katika kuthibitisha manunuzi yaliyofanywa kwenye mwaka husika wa mapato ili kuhimiza utoaji risiti za kielektroniki na kulinda mapato ya Serikali. Aidha, hatua hii haitahusisha muuza bidhaa au mtoa huduma ambaye ni raia wa kigeni na hayupo Tanzania au mtu yeyote ambaye hayupo katika wigo wa kutoa risiti za kielektroniki.

### c. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147

i. Serikali imepunguza ushuru wa bidhaa kwenye kila lita ya maji ya kunywa yaliyosindikwa kwenye chupa yanayozalishwa nchini kutoka shilingi 63.80 kwa lita hadi shilingi 56 kwa lita ili kuchochea ukuaji wa viwanda vidogo vinavyozalisha maji nchini, kupunguza gharama kwa walaji na kuchochea matumizi ya maji safi na salama;

ii. Serikali itatatoza ushuru wa bidhaa kwenye uzalishaji wa vilevi kwa kiwango cha shilingi 7,000 kwa kila lita ya *un-denatured ethyl alcohol* yenye kilevi cha asilimia 80 au zaidi inayotoka nje ya nchi, na shilingi 5,000 kwa kila lita ya *un-denatured ethyl alcohol* yenye kilevi cha asilimia 80 au zaidi inayozalishwa ndani ya nchi. Utozaji huo hautahusisha *un-denatured ethyl alcohol* inayotumika kwa matumizi mengine yasiyohusu uzalishaji wa vilevi baada ya kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ya masuala husika;

iii. Serikali itatoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye ada ya matangazo ya biashara za

michezo ya kubahatisha na bahati nasibu ya Taifa yanayotangazwa kupitia vituo vya televisheni, redio, na tasnia ya uchapishaji ili kuongeza wigo wa kodi;

iv. Kuanzisha ada ya shilingi 30,000 ya usajili wa vituo vya bahati nasibu ili kuongeza ufanisi na udhibiti bora wa michezo ya kubahatisha;

v. Serikali itatoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha shilingi 300 kwa kilo ya *tomato sauce* na *tomato ketchup* pamoja na *chilli sauce* na *chilli ketchup* zile zinazotoka nje ya nchi ili kuongeza mapato ya Serikali na kupata fedha za fidia ya athari hasi zinazotokana na matumizi ya sukari na chumvi iliyopo katika bidhaa hizo;

vi. Serikali itatoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha shilingi 500 kwa kilo moja ya rangi za mafuta zinazotoka nje ya nchi ili kuongeza mapato ya Serikali na kupata fedha za fidia ya athari hasi zinazotokana na matumizi ya bidhaa hizo;

vii. Serikali itatoza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha shilingi 963.90 kwa lita ya bia isiyochujwa, mfano wa Kibuku na shilingi 2,959.74 kwa lita ya pombe zenye mchanganyiko wa matunda zinazoingizwa kutoka nje ya nchi, ili kuleta usawa katika utozaji kodi; na

viii. Serikali imeelekeza kuwa, asilimia 2 ya mapato ya ushuru wa bidhaa yanayokusanywa kutoka kwenye bidhaa za urembo, vinywaji laini na vileo (bia na pombe kali) kupelekwa kwenye Bima ya Afya kwa wote ili kuongeza fedha zitakazotumika kwa ajili ya kugharamia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo na makundi maalum hususan wanawake wajawazito na watoto wa umri chini ya miaka mitano.

Hatua hizi za ushuru wa bidhaa kwa ujumla wake zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 196.14.

### d. Sheria ya Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Mwaka 2018

Serikali imefanya maamuzi ya muda mfupi ya kugharamia malipo ya nyongeza ya mkupuo kwa asilimia 7 kwenye kikokotoo ili kufikia asilimia 40 kwa kundi ambalo lilikuwa linalipwa asilimia 50 kabla ya kuunganishwa kwa mifuko ya pensheni. Vile vile, imeongeza kikokotoo kwa asilimia 2 ili kufikia asilimia 35 kwa kundi ambalo lilikuwa linalipwa asilimia 25 kabla ya kuunganishwa kwa mifuko ya pensheni. Nyongeza hizo zitaanza kulipwa kwa wastaafu waliostaafu kuanzia mwaka 2022/23 na kuendelea hadi watakaostaafu mwaka 2029/30 na baada ya hapo mfuko wa PSSSF utachukua jukumu la kuendelea kuwalipa

mafao. Lengo la hatua hii ni kutoathiri mfumo mzima wa pensheni kwa kuwa na uwiano wa mafao kwa wanachama na kuupa Mfuko muda wa kuangalia uhimilivu wake.

Hatua hii inatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 155.40.

**e. Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004**

i. Serikali itatoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 35 badala ya asilimia 10 kwenye vioo vya kawaida na vigumu kwa mwaka mmoja ili kulinda wazalishaji wa vioo wa ndani;
ii. Serikali imeongeza ushuru wa forodha wa asilimia 35 au dola za Marekani 3.0 kwa kila mita moja ya mraba kwa mwaka mmoja kwenye marumaru ili kulinda viwanda vya ndani;
iii. Serikali itatoza ushuru wa forodha kwenye bidhaa za chuma kama vile mabati, nondo na misumari ili kulinda viwanda vya ndani na kuongeza ajira;
iv. Serikali itatoza ushuru wa forodha kwa kiwango cha asilimia 50 badala ya 35 kwenye chumvi inayotumika nyumbani kwa mwaka mmoja ili kulinda wazalishaji wa ndani;

Hatua zote kwenye ushuru wa forodha kwa ujumla wake zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 205.72.

**f. Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, SURA 196**

Kutoza ushuru kwa kiwango cha asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya kula ya alizeti, mashudu yanayotokana na mbegu za alizeti pamoja na mbegu za alizeti zinazosafirishwa kwenda nje ya nchi. Lengo la hatua hii ni kuwezesha upatikanaji wa bidhaa za mafuta kwa bei nafuu nchini pamoja na kulinda wazalishaji wa ndani kwa kuhakikisha wanapata mbegu za alizeti za kutosha ambazo zinatumika kama malighafi katika viwanda hivyo.

Hatua hizi kwenye Sheria ya usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi kwa ujumla wake zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 2.04.

## MGAWANYO WA MATUMIZI KISEKTA KWA MWAKA 2024/25

Shilingi Milioni

| SEKTA | KIASI |
|---|---|
| **1 - Elimu** | **6,168,388.76** |
| 1.1 - Elimu Msingi | 4,395,264.03 |
| 1.2 - Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi | 196,535.15 |
| 1.3 - Elimu ya Juu | 1,347,027.99 |
| 1.4 - Sayansi, Teknolojia na Ubunifu | 72,373.38 |
| 1.5 - Huduma za Utawala | 157,188.21 |
| **2 - Afya** | **2,540,886.36** |
| 2.1 - Huduma za Tiba | 1,062,378.46 |
| 2.2 - Huduma za Kinga | 310,732.26 |
| 2.3 - Hospitali za Rufaa za Mikoa | - |
| 2.4 - Zahanati | 61,016.70 |
| 2.5 - Vituo vya Afya | 109,278.62 |
| 2.6 - Hospitali za Wilaya | 901,820.69 |
| 2.7 - Huduma za Utawala | 95,659.63 |
| **3 - Huduma za Utawala na Deni la Serikali** | **13,237,705.96** |
| 3.1 - Utawala na Bunge | 5,068,045.52 |
| 3.2 - Usimamizi wa mapato na Matumizi | 2,346,935.97 |
| 3.3 - Mambo ya Nje na Ushirikano wa Kimataifa | 240,751.29 |
| 3.4 - Deni la Serikali (Malipo ya Riba) | 5,581,973.18 |
| **4 - Ulinzi, Utawala wa Sheria na Usalama** | **5,493,173.75** |
| 4.1 - Ulinzi | 3,323,461.85 |
| 4.2 - Usalama wa Umma | 1,703,820.40 |
| 4.3 - Mahakama | 465,891.50 |
| **5 - Maendeleo ya Uchumi** | **10,291,020.55** |
| 5.1 - Kilimo | 1,938,941.21 |
| 5.2 - Madini | 231,908.91 |
| 5.3 - Nishati | 1,883,743.06 |
| 5.4 - Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano | 5,483,920.50 |
| 5.5 - Maliasili, Utalii na Mazingira | 335,351.53 |
| 5.6 - Viwanda | 111,148.03 |
| 5.7 - Biashara | 272,012.78 |
| 5.8 - Kazi, Maendeleo ya Vijana na Kukuza Ujuzi | 33,994.53 |

Shilingi Milioni

| SEKTA | KIASI |
|---|---|
| **6 - Hifadhi ya Jamii** | **2,653,438.56** |
| 6.1 - Wazee, Watoto na Watu wenye Ulemavu | 50,109.80 |
| 6.2 - Mifuko ya Hifadhi ya Jamii | 2,157,073.96 |
| 6.3 - Mfuko wa Bima wa Afya | 446,254.80 |
| **7 - Maji, Makazi na Maendeleo ya Jamii** | **1,421,581.00** |
| 7.1 - Maji | 641,882.33 |
| 7.2 - Ardhi, Nyumba na Makazi ya Watu | 174,091.59 |
| 7.3 - Maendeleo ya Jamii | 320,316.13 |
| 7.4 - Habari, Michezo na Utamaduni | 285,290.96 |
| **Jumla ya Sekta** | **41,806,194.94** |
| | |
| Deni la Serilaki (Malipo ya Mtaji) | 7,539,492.63 |
| | |
| **Jumla Kuu** | **49,345,687.56** |